


KUANGALIA YASIYOONEKANA

 Inaonekana ni vyema kurudi katika nyumba ya Bwana, usiku wa leo, baada ya usiku mzuri sana kama ilivyokuwa jana usiku. Nasi tulikuwa na wakati mzuri sana, siku hizi mbili au tatu zilizopita usiku humu jengoni, nasi tunamshukuru Baba yetu wa Mbinguni kwa hilo. Nafsi zimezaliwa katika Ufalme wa Mungu. Na taarifa nzuri sana kutoka kwa huduma za uponyaji!

² Nasi tumepata habari muda mfupi tu uliopita, ya kwamba yule msichana aliyetoka mahali fulani hapa juu, katika mji fulani, aliyekuwa na leukemia, wakati. . . alitangazwa amepona, leo, na daktari wake, kwamba hu—huyo mtoto ni mzima. Uhuhuh. Nao. . . Alikuwa awe mmishenari. Mnakumbuka kisa hicho. Na—naye Shetani alikuwa akijaribu kumnyang'anya hilo. Naye ametangazwa kuwa mzima na mwenye afya, kutoka kwa daktari wake.

³ Naye yule mhudumu kipofu aliyekuwa hapa apate kuona, na wengine! Na kuna mambo makuu tu ambayo Bwana anafanya.

⁴ Sasa, jana jioni nilichukua kundi kwenye chumba cha maombi humu ndani, nipate tu kuona kama ile huduma mpya iliyoahidiwa ingeanza humu maskanini, kabla hatujapiga ile hema. Vema, sasa, ni juavyo mimi, hapakuwapo na kitu zaidi ya ninii tu. . . Mara tu nilipoingia mle, Roho wa Bwana akaingia, Naye akaanza tu kuzipambanua roho, na kuwaambia watu shida zao na kadhalika.

⁵ Lakini, nashangaa. Niliwauliza hao watu, kama kulikuwa na uwezekano wowote kwao kukaa. Ningependa tu kuwauliza ikiwa kumekuwa na mabadiliko ndani yao. Ikiwa wanajisikia kwamba wameponywa, au mabadiliko yoyote yanayoonekana kwa njia yoyote; niliwauliza, usiku wa leo, kama ningewaita, kama wangeweza kuingia jengoni, ningependa wainue mikono yao. Sasa, kama wako hapa, wala haikuwalazimu kwenda nyumbani, wote walikuwa watu wa nje ya mji. Na kama hawakulazimika kwenda nyumbani, na wameingia humu jengoni, na unaona kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa, tafadhali inua mkono wako. Wale, ambao, kama kuna yeyote hapa aliyekuwa jengoni jana usiku, aliyembewa hapa nyuma. Kwa vile sioni mikono yoyote, sijui kama hao watu wangeweza hata kukaa.

⁶ Pale, mmoja, mmoja nyuma hapa. Vema. Mmoja pale. Vema, hilo ni zuri sana. Unahisi ya kwamba kumekuwa na badiliko, sivyo, bwana, wewe uliyeinua mkono wako? [Ndugu mmoja anasema, “Naam. Nimekuwa macho, siku nzima.”—Mh.] Vema, hilo ni jema. [“Ninainama. Sijawa na haja ya dawa kwa ajili yake, siku nzima, ama, vema, jana usiku.”] Sisi. . . Hilo ni

zuri sana, na tunashukuru. Hakukuwa na kitu kinachoonekana ambacho tungeweza kuona, unaona. Kwa sababu. . .

⁷ Na kulikuwa na mwa—mwanamke chumbani, ambaye alikuwa na matatizo ya akilini. Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kunena naye, na kumwambia mambo yaliyokuwa yamefanywa. . . yaliyokuwa yametokea maishani mwake, ambapo alifikiri kwamba jambo fulani lilikuwa limempata, ambalo halikuwa limempata. Nami nadhani, kama ndugu yetu, yule aliyepo, ambaye anajua hilo. Na ndipo ikaanza kumwambia juu ya mtu aliyekuwa na ndevu ndefu, na nywele ndefu, alikuwa amemwomba. Alikuwa tayari. . . amesahau, akasema, “Hapana.” Ndipo basi kuonyesha usahihi na ukamilifu wa Roho Mtakatifu, alirudi tena, na kumchukua huyo mtu, na kuwaambia ilikuwa ni nani, na mahali lilipotokea. Ndipo akasema, “Nakumbuka sasa.” Hiyo ilikuwa miaka mingi iliyopita. Jinsi ambavyo ukamilifu wa Roho Mtakatifu! Loo, Yeye ni halisi sana!

⁸ Sasa, tumesongamana, na mkutano huu mdogo tu hapa, kabla tu sijaondoka tena. Nami nilikuwa na furaha sana usiku wa leo, kukutana, nilipokuwa nikiingia tu, na rafiki wa zamani, Ndugu Rogers, kutoka huko Milltown, Indiana. Na marafiki ambao sijawaona kwa miaka. Ndugu Creech tena, alikuwa hapa jana jioni.

⁹ Na leo hii, katika mahojiano, Roho Mtakatifu alikuwa mzuri sana, leo. Na inaonekana kana kwamba itaendelea tu kwa muda, mpaka hema hiyo iingie, chini ya huduma ile ile ambayo nimekuwa nayo. Kwa sababu, katika mahojiano leo, kulikuwa na maono manne makuu yaliyotukia, katika mahojiano. Kwa hivyo, inaonekana, labda, nitaendelea hadi ambapo labda hiyo hema itaanza, ama popote pale Yeye amechagua kuanza kulitangaza Jina Lake kwa njia mpya. Lakini itakapotokea, itakuwa kamilifu tu kama hizo zingine. Itakuwa tu. . . Nami ninatumaini kwa Mungu kwamba itakuwa kubwa zaidi kuliko zile zingine. Si kwa sababu ya—ya huduma yetu, lakini kwa ajili ya wagonjwa na wahitaji. Kuna haja kubwa sana nchini siku hizi!

¹⁰ Sasa tutaingia moja kwa moja kwenye Neno, na ili wale wanaosimama isiwabidi kusimama kwa muda mrefu sana. Sasa, kwanza, kabla hatujasoma Neno Lake, hebu na tuzungumze Naye kibinafsi, tunapoinamisha vichwa vyetu.

¹¹ Mungu Mpendwa, tunakuja katika Uwepo Wako mtakatifu sasa, kwa mioyo minyenyekevu na vichwa vilivyoinamishwa. Nasi tunakuomba utusamehe jambo lolote ambalo huenda tumefanya, ama—ama kuwazia, au kusema, katika siku hii, ambalo limekuwa kinyume na Mapenzi Yako. Tungeomba kwamba ungetusamehe kila mmoja wetu kwa neema.

¹² Na tumekusanyika usiku wa leo si kwa madhumuni mengine ila kukuabudu Wewe, na kuelezea hisia zetu na ibada ya mioyo

yetu Kwako. Nasi tuna hakika, Bwana, ya kwamba kusanyiko hili dogo ambalo limesongamana kwenye maskini kuta hizi ndogo usiku wa leo, halijakuja hapa kuonekana. Hawakuja hapa kwa kusudi lingine ila kuonyesha upendo wao Kwako. Hawangesimama nje kuzunguka madirisha, na kuzunguka kuta, huku viungo vyao vikiuma, ili tu kuonekana. Wapo hapa kwa sababu wanaamini, kwamba, “Wewe upo, na huwapa thawabu wale wakutafutao kwa bidii.”

¹³ Tungeomba msamaha wa dhambi zote za watu. Na Nguvu za uponyaji ziletwe juu ya wagonjwa na wahitaji. Nasi tunakuomba ulibariki Neno Lako, Bwana, tunapolisoma. Hatufai kutafsiri Neno hili. Kwa hiyo naomba Roho Mtakatifu aje, na kuingia moja kwa moja katika Neno, na kulitia ndani kabisa mioyoni mwa watu. Na jalia, kupitia hili, kuwe na mavuno mengi ya nafsi na ibada kuu ya uponyaji. Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunaomba haya kwa unyenyekevu katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁴ Kwa usomaji wa Maandiko, usiku wa leo, ningependa kusoma kutoka katika Kitabu cha Wafalme wa Pili, kuanzia kifungu cha 8. Na somo langu usiku wa leo ni: *Kuangalia Yasiyoonekana*.

¹⁵ Usiku wa kwanza, nilikuwa nikihubiri juu ya somo la: *Kumwinua Kutoka Katika Historia*. Na usiku wa pili, jana usiku, nilikuwa nikihubiri juu ya somo: *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*.

¹⁶ Na, usiku wa leo, somo langu ni: *Kuangalia Yasiyoonekana*. Sasa, Wafalme wa Pili, mlango wa 6, kuanzia kifungu cha 8.

Basi, mfalme wa Shamu alikuwa akifanya vita na Israeli, akafanya mashauri na watumishi wake, akasema, Kituo chetu kitakuwa mahali fulani.

Yule mtu wa Mungu akapeleka habari kwa mfalme wa Israeli, kusema, Jihadhari usipite mahali fulani; kwa sababu ndiko watakaposhukia Washami.

Mfalme wa Israeli akapeleka watu wake mahali pale alipoambiwa na yule mtu wa Mungu, na kuhadharishwa, akajiokoa nafsi yake, si mara moja, wala si mara mbili.

Basi mfalme wa Shamu moyo wake ukamfadhaika sana kwa ajili ya jambo hili; akawaita watumishi wake, akawaambia, Je, hamtanionyesha ni mtu yupi miongoni mweni aliyepande wa mfalme wa Israeli?

Mmojawapo wa watumishi wake akasema, La, bwana wangu, Ee mfalme, ila Eliya, yule nabii aliye katika Israeli, yeye humwambia mfalme wa Israeli maneno unenayo katika chumba chako cha kulala.

Akasema, Enendeni mkamwangelie alipo, nipate kupeleka watu kwenda kumchukua. Akaambiwa ya kwamba yuko Dothani.

Kwa hiyo akapeleka farasi huko, na magari, na jeshi kubwa: wakafika usiku, wakauzingira mji ule pande zote.

Hata asubuhi na mapema mtumishi wake yule mtu wa Mungu alipoondoka na...-kapita mji...farasi na magari. Mtumishi wake akamwambia, Ole wetu, bwana wangu! tutafanyaje?

Akajibu, Usiogope, kwa maana walio pamoja nasi... wengi kuliko... walio pamoja nao.

Eliya akaomba, akasema, Ee BWANA, nakusihii, fungua huyu...mfumbue macho yake, apate kuona. BWANA akamfumbua macho yule mtumishi; naye akaona: na tazama, vilima vilikuwa vimejaa farasi na magari ya moto...kumzunguka Eliya pande zote.

¹⁷ Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

¹⁸ Ni ajabu kwamba mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, na aliitwa Naye kutembea kwa imani, akiamini kwamba Mungu yuko, angechagua kutembea kwa kuona badala ya kwa imani; baada ya umbo lake, utu wake, na yote yaliyomo ndani yake kuumbwa kwa sura ya Mungu. Naye Mungu ni yule Yehova mkuu Ambaye huita vile vitu ambavyo havikuwepo, kana kwamba vilikuwako. Naye mwanadamu, aliyeumbwa kuishi na Mungu namna hii, hata hivyo amechagua kutembea kwa kuona kwake. Anataka kuwa bosi wake mwenyewe. Hataki mtu yeyote amwambie cha kufanya. Hiyo ni tabia ya mwanadamu tu. Ilihibitika kuwa hivyo katika bustani ya Edeni, alipokuwa amepoteza ushirika wake na Mungu, kwa kuchagua kufuata njia yake mwenyewe, asiwe na mtu atakayemtawala.

¹⁹ Lakini mwanadamu ameumbwa kama kondoo. Na kondoo hawezi kupata njia ya kurudi, naambiwa. Anapopotea, amepotea kabisa. Na hivyo ndivyo ilivyo na mwanadamu. Akipotea, hajiwezi kabisa. Ni lazima awe na mchungaji wa kumwongoza.

²⁰ Naye mwanadamu anapochagua, kadiri siku zinavyosonga mbele, tunamwona mwanadamu akiendelea kuwa mbaya zaidi, akiona heri atembea kwa kuona kuliko kwa imani, kwa Yasiyoonekana. Na anapofanya hivyo, anamnyang'anya mtu wa ndani, ambaye ni nafsi. Na hiyo ndiyo sehemu ya Milele ya mwanadamu.

²¹ Sasa, "Mtu hataishi kwa mkate tu," alisema Bwana, "bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

²² Na utu wa kimwili wa mwanadamu, ulio wa kutunzwa, sio sababu pekee ya Mungu kumweka duniani, kwa sababu anachofanya na mwili huu hufaidi kidogo sana. Ni nafsi yake, ndiyo muhimu. Ni mtu wa ndani, ambaye hakutoka duniani. Alitoka Mbinguni, na hiyo ndiyo sehemu ya Milele ya mwanadamu.

²³ Lakini, hata hivyo, ni ajabu kwamba anajaribu kujitafutia njia yake mwenyewe ya kutoka. Nasi tunaona hivyo katika Maandiko, kwamba, mtu anapochagua kutembea katika njia yake mwenyewe na kufanya jinsi anavyotaka, Mungu huachana tu na yeye.

²⁴ Mwanadamu hapaswi kujiwazia mwenyewe, bali aache nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yake. Hatupaswi kujiwazia. Tunapaswa kuita chochote kinyume na kile alichosema kana kwamba sivyo. Haijalishi macho yetu yanadai kuwa nini, hatuishi kulingana na kile tunachona. Tunaishi kwa kile tunachoamini.

²⁵ Siku chache zilizopita, nilikuwa nikisikiliza kipindi kwenye redio, nikija kwenye shule ya Jumapili, na ulikuwa ni mjadala wa mezani, pamoja na matineja, huko Louisville. “Mojawapo ya mambo muhimu zaidi lilikuwa ni gani? Ni msichana kumpata mvulana mwenye nywele za mawimbimawimbi; au, mvulana, msichana mwenye macho mazuri ya bluu au kahawia? Je, hilo lilileta tofauti?” Inaonekana kwamba hilo lingekuwa jambo kuu kwa tineja. Lakini hilo silo jambo muhimu zaidi.

²⁶ Jambo muhimu kuliko yote ni kwamba, mtafute Mungu wako, Muumba wako. Usichanganyishe ndoa. Olewa na mvulana anayeamini hasa kama wewe unavyoamini. Kwa maana, hata hivyo, Mungu ndiye jambo muhimu ambalo tuko duniani kufanya, ni kumtumikia Yeye. Na kama ukioa ama chochote kinyume na Hilo, utalipia katika siku zilizo mbele yako. Lazima ukumbuke kila mara, “kwa imani,” wala si kwa kuona. “Mwenye haki ataishi kwa imani.” Nasi tunatazama Yasiyoonekana.

²⁷ Nasi tunaweza kuendelea kwa saa kadhaa, tukizungumza juu ya siku ya kisasa, jinsi wanaume na wanawake, siku hizi, wanavyoangalia tu kabisa. Nao wanashuka mtaani, na watachagua kanisa ambalo hawana budi kuhudhuria, na kuwalelea watoto wao. Nao watatafuta kote mjini, bila kujaribu kupata kanisa la kiroho zaidi, bali kanisa kubwa zaidi wanaloweza kupata, lile ambalo lina u—u—umati mkubwa zaidi, na waliovalia nadhifu zaidi, na watu mashuhuri wa mji wanahudhuria kanisa hili, ambamo wanaitwa “wa tabaka bora,” kadiri wanadamu wajuavyo. Na halafu, katika kanisa hilo, watajaribu kutafuta mhudumu ambaye, kile wanachoita, “asiye na akili finyu,” ambaye atawaacha tu waishi vyovyote watakavyo, na kuwa wafuasi wa kanisa hilo.

28 Lakini mtu wa kiroho, kwa ndani, kama utampa uhuru wa kujichagulia, huenda akakuongoza kwenye misheni ndogo mahali fulani, ambapo hakuna watu wengi, lakini pana Roho wa Mungu aliye hai. Kwa maana, mtu wa nje hula saikolojia na mambo ya kiakili, bali mtu wa ndani hula Neno la Mungu.

29 Na sasa kama tukifungua, katika Biblia zetu, kwa wengi wa wahusika wa Maandiko, ingetuchukua saa nyingi kuwapitia. Lakini hebu na tufikirie tu juu ya Kitabu cha Waebrania, mlango wa 11, kwa dakika chache. Nasi tunasoma hapa, ya kwamba Ibrahimu, alikuwa mwanadamu tu, naye aliishi katika mji wa Uru katika nchi ya Wakaldayo. Na mtu wa kawaida tu wa kutembea kila siku, lakini siku moja akakutana na Mungu. Naye Ibrahimu akabadilishwa, tangu siku hiyo na kuendelea. Haidhuru alihudhuria kanisa lake vizuri jinsi gani, kanisa la baba yake, lakini, mara alipokutana na Mungu, alikuwa mtu aliyebadilika.

30 Nami ninaamini kuwa hiyo haijakoma kuwepo hata wa leo. Mtu anaweza kuwa mshiriki mwaminifu wa kanisa. Anaweza kuwa anatembea kiadilifu mbele ya jirani yake na familia yake, lakini, anapokutana na Mungu, yeye ni mtu aliyebadilika.

31 Siku moja, ninakumbuka nikizungumza na mtu msomi, ambaye alisema, “Utajuaje kuwa kuna tofauti yoyote na kile ambacho dini yoyote inaweza kutoa?”

32 Nikasema, “Nilisoma, katika Biblia, juu ya Mungu aliye hai. Nikasoma juu ya wema Wake. Nikasoma juu ya subira Yake na Nguvu Zake. Nami niliamini hilo kama vile tu mtu yeyote angeweza kuamini. Lakini siku moja nilikutana na Yule niliyesoma habari zake, ndipo kukatokea mabadiliko ya ghafla. Na sijawahi kuwa vile vile tangu wakati huo, na natumaini sitakuwa.” Kitu fulani kinafanyika. Wakati kuona kunashindwa kuleta, imani iko pale kushika mahali hapo na kuileta.

33 Nasi tunaona ya kwamba, Ibrahimu, yeye hakuwa kijana wakati jambo hili lilipotukia. Alikuwa mzee, mwenye umri wa miaka sabini na mitano. Na mkewe, Sara, ambaye alikuwa dada yake wa kambo; nao walikuwa wameoana miaka mingi, mingi sana, tangu alipokuwa msichana wa miaka kumi na saba hivi, inaaminiwa. Ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu, “Nimekuchagua wewe pamoja na Sara, kwamba mtapata mtoto.” Naye Sara alikuwa tasa, maishani mwake mwote. Lakini Ibrahimu kamwe hakuangalia yale macho yake yangeona, mwanamke mzee mwenye makunyanzi, amepita wakati wa maisha kwa miaka mingi, kupata watoto, lakini aliangalia Yasiyoonekana, naye akamwona Isaka. Kwa imani alimwona Isaka. Naye, baada ya kuangalia Yasiyoonekana, “Aliviita vitu ambavyo havikuwako, kana kwamba vilikuwako.” Akapata mtazamo wa yale Yasiyoonekana. Kwa imani akayaona. Nayoi

Biblia inasema, kwamba, “Alivumilia, kana kwamba anamwona Mungu asiyeonekana akiwa pamoja naye,” kote safarini.

³⁴ Wakati mtu anapopata ono hilo la Mungu asiyeonekana, na kujua ya kwamba Yeye daima yuko, kuna kitu ambacho huimarisha mawazo ya mtu huyo. Huimarisha matendo yake. Na wakati wa dhiki na taabu, bado kitamfanya aangalie juu na juu ya mambo yanayotukia karibu naye, kwa sababu anatazama Yasiyoonekana, hata hivyo, kwa ahadi.

³⁵ Sasa, jinsi Ibrahimu, sio tu kwamba aliona Yasiyoonekana. . . Na sababu ya kuamini jambo hilo, ilikuwa ni kwa sababu Mungu alisema hivyo. “Na kama sisi tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Na kama Roho aliyekuwa ndani ya Kristo anakaa ndani yetu, anafanya jambo lile lile. Anachukua kila ahadi ya Kiungu ya Mungu iliyo katika Biblia Yake, na kuiita wakati uliopo, na kujituliza Mwenyewe hapo.

³⁶ Ambapo, ukiangalia, kwa macho yako, na uone sasa kwamba taifa letu linatetemeka na kutikisika. Mawingu ya vita yanaruka kila mahali; kila taifa liko chini ya dhiki na fadhaa ya wakati. Kila ishara, ambayo Yesu alisema ingetukia, inatukia. “Kungekuwa na ishara mbinguni juu na katika nchi chini.” Na mambo makuu yangukuwa yakitukia, kama vile visahani virukavyo na mambo ya kushangaza yakitukia.

³⁷ Lakini aliliamuru Kanisa Lake kuinua vichwa vyao, katika siku hiyo, na kuangalia juu, kwa maana Kristo asiyeonekana atatokea hivi karibuni. Kwa hivyo ikiwa tunatembea tu kwa kuona, tungekuwa watoto wa giza, hakika kabisa sasa. Lakini nina furaha sana kujua ya kwamba kuna Nuru inayoangaza katika moyo wa kila mwaminio, mpaka ile Siku ya Milele Yesu atakopokuja.

³⁸ Sasa ni funzo kwetu, kuangalia kile Ibrahimu alichofanya. Na kisha si kwamba aliamini tu, bali alijiandaa kwa ajili yake. Alifanya maandalizi kwa ajili ya. . . mtoto huyu ambaye alimwona kwa imani, miaka ishirini na mitano kabla mtoto huyo hajaja. Kwa sababu, alikuwa amezingatia ya kwamba Yeye aliyemwambia, aliweza kutimiza ahadi ambayo Yeye alikuwa amemwambia. Hakuzingatia utu wake wowote, akiwa na umri wa miaka mia moja, mwili wake, wala hakuzingatia, hata kidogo, kufa kwa tumbo la uzazi la mkewe, Sara. Naye mwandishi wa maoni ya Kiungu anatwambia, kwamba, “Hakusita kwa ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu.” Ni mtu wa jinsi gani!

³⁹ Na, leo hii, hakuna haja, hakuna haja ya hata kujaribu kulikaribia kwa imani ya kiakili. Hutaweza kamwe kufanya hivyo. Utaenda kutoka kanisa moja hadi kanisa lingine, na kutoka mstari wa maombi hadi mstari wa maombi, wala usipate kamwe. Huna budi kufika mahali ambapo limetatuliwa

Milele, mara moja. Ama Yeye ni Mungu, au Yeye si Mungu. Ninawahurumia watu; kama nilivyokuwa nikizungumza jana jioni.

⁴⁰ Naye Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi.” Nao Mzabibu ukazaa tawi la kwanza. Nalo hilo tawi la kwanza lilikuwa pentekoste, na baraka za kipentekoste zimeandikwa katika Kitabu cha Matendo. Na kama tawi la kwanza lilikuwa pentekoste, tawi la pili itabidi liwe pentekoste. Na itabidi lizae aina ile ile ya Kanisa na tabia ambayo tawi la kwanza lilizaa.

⁴¹ Je, Yesu hakuzungumza jambo hilo katika Yohana Mtakatifu 14, aliposema kwamba tawi lisilozaa litakatwa, litanyauka? Hapo ndipo madhehebu yetu ya siku hizi yalipo, yatapogolewa kutoka kwa ule Mzabibu.

⁴² Ni lile tu lenye kuzaa matunda, aina ile inayozaa matunda na kazi za Roho Mtakatifu, itaweza kuendelea katika huo Mzabibu. Kwa maana, Uhai ulio katika Mzabibu huo, huchipuza katika tawi. Nao Uhai uliokuwa ndani ya Yesu, ulikuwa katika lile Kanisa la kwanza. Nao hawakutembea kwa kuona. Walitembea kwa imani, wakiamini yale Mungu aliyosema yalikuwa Kweli. Loo, ni tofauti ya jinsi gani, wakati watu ambao watatembea kwa imani, na kuita chochote kilicho kwa kuona, ambacho ni kinyume cha Neno, kana kwamba hakikuwepo. Tunahitaji aina hiyo ya imani Kanisani.

⁴³ Musa, alipokuwa na umri wa miaka arobaini, kijana mwanamume, na, kadiri ilivyoonekana kwa macho, Musa alishika ulimwengu mkononi mwake. Alikuwa halifa wa farao wa Misri. Naye alishika nchi zote ulimwenguni, moja kwa moja mkononi mwake, awe mfalme juu ya dunia nzima, iliyojulikana siku hizo. Na, hata hivyo, alichungulia kupitia dirisha ambalo Farao alichungulia, naye akawaona hao Waebrania.

⁴⁴ Kwa Farao, aliyewatazama, hawakuwa chochote ila kundi la wakanyaga matope, huko chini matopeni, wakitengeneza matofali. Kwa watu mashuhuri, walipopitia pale, walikuwa vivyo hivyo. Watu waliovalia vizuri, “Hilo lilikuwa ni kundi la watumwa; si kitu ila watu wanaogaaga matopeni.”

⁴⁵ Lakini Musa alipochungulia kwenye dirisha lile lile, aliwaona vinginevyo, kwa sababu aliangalia Yasiyoonekana na kujua kwamba Mungu aliahidi ya kwamba angewakomboza kutoka mahali hapo, na kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi. Kwa kuwa aliangalia Yasiyoonekana. Aliona miaka ambayo ilikuwa inakuja, mbele. Akaona Misri ikiharibiwa, ingawa ilikuwa katika wakati wake wa ufanisi. Aliiona Misri kama ilivyo siku hizi. Kisha akawaona Israeli wote wameketi raha mstarehe wamemzunguka Ibrahimu, Utukufuni. Na kwa imani akachagua kuchukua ma—mabaya kuliko yote dini ingeweza kumpa, na kulinganisha na yaliyo bora kuliko yote ambayo ulimwengu ungeweza kumpa. “Naye alichagua kuteseka kwa

shutuma za Kristo, na aliiona kuwa ni hazina kubwa kuliko yale yote Misri ingeweza kumpa. Kwa maana alistahimili, kama amwonaye Yeye asiyeonekana. Mungu alikuwa amezungumza na Musa, na Musa alijua Mungu alikuwa ni Nani. Kwa hivyo, hakuangalia mng'ao.

⁴⁶ Na hapa naweza kuliambia kanisa usiku wa leo. Musa alishika, kwa mkono mmoja, yaliyo bora kuliko yote ulimwengu ungeweza kumpa. Kusungekuwa na bora zaidi. Ulikuwa ndio wadhifa wa juu zaidi. Yalikuwa ndiyo bora sana ulimwengu uliyokuwa nayo. Nayo dini ikampa mabaya kuliko yote ambayo yangeweza kutolewa, kundi la watumwa kwenye shimo la matope. Na sasa, kama mtu alikuwa akiangalia, angechukua upande gani?

⁴⁷ Hebu niseme jambo hili kwa unyofu, na bila ubaya wowote, lakini hebu niseme hivi ili mwelewe. Siku hizi, usiangalie kanisa kubwa. Usiangalie dhehebu kubwa. Usiangalie waliovaa vizuri. Lakini mwangalie Kristo, ambaye alikuwa tajiri na akawa maskini, ili kwa umaskini Wake mpate kufanywa matajiri. Na unapotafuta kanisa, usiende ambapo watu wote mashuhuri huenda, ama ma-Ph.D. wakubwa, ama ma-D.D., bali waangalie watu wanaodharauliwa.

⁴⁸ Naye Musa, alipokuwa ameyashika kwa mikono yote miwili, yaliyo bora kuliko yote ulimwengu ungeweza kutoa, na yale angeweza kuona. Na hata hivyo, alipoangalia Yasiyoonekana, mabaya zaidi ambayo kanisa lingeweza kumpa, alichagua kutembea kwa imani. Naye akachagua kutembea kwa Yasiyoonekana, Mungu, akihesabu kuwa ni hazina kuu kuliko yote ambayo macho yake yangeweza kumwonyesha. Huu hapa ufalme, huu hapa utawala, hiki hapa kiti cha enzi, hii hapa taji, hapa alikuwa na kila kitu, mkononi mwake. Lakini, hata hivyo, kwa imani, alipopata mtazamo wa mara moja wa Kristo huko nje kwenye mashimo ya matope, aliwaendea watu wake.

⁴⁹ Sasa, hili hapa somo lingine dogo juu ya Musa. Sasa, Musa hakuketi tu nyuma na kusema, "Nawahurumia watu hao. Hao ni watu wema. Unajua, nisingesema neno moja dhidi yao."

⁵⁰ Sasa, hivyo ndivyo wanadini wengi wanavyofanya siku hizi, wanaposikia ujumbe mkali kuhusu Mungu halisi. Watasema, "Loo, sina lolote dhidi ya hao watu wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu. Sina chochote dhidi ya wale watu wanaoamini miujiza." Lakini hiyo haitoshi.

⁵¹ Musa hakuwahurumia tu, na kubakia kwenye kiti cha enzi. Alitoka akawa mmoja wao.

⁵² Nami nakumbuka, miaka michache iliyopita, nilipokuwa na ahadi kuu na Wabaptisti. Halafu Wapresbiteri, mama mmoja wa mji huu alikuwa akilipia mafunzo yangu ya shule fupi katika dhehebu la Presbiteri, nao walitaka kunichukua kama mhudumu. Lakini nilipoangalia huko nje na kuona ya kwamba

lile kundi lililoamini katika mambo ya kimbinguni lilichekwa na kuitwa “watakatifu wanaojibingirisha,” ilikuwa ni rahisi kuendelea, mhubiri wa Kibaptisti, kwa maana nilikuwa mmoja. Lakini badala ya kuwaangalia na kusema, “Loo, sina neno dhidi yao. Naamini hilo, pia,” nilichagua kuwa mmoja wao; nikatoka nje.

⁵³ Na sasa mimi ni mmoja wa wale wanaoitwa “watakatifu wanaojifingirisha,” kwa sababu ninaona mle ndani, wanayo ishara ya Mungu aliye hai anayeishi pamoja nao, na kwa imani ninaamini ya kwamba hilo ndilo kundi litakalokwenda katika Unyakuo. Na ni heri niwe Nalo kuliko ma-Ph.D. na ma-D.D. yote ambayo ulimwengu wa kanisa ungeweza kumudu. Usiwahurumie. Kuwa mmoja wao. Hapo ndipo, kwa imani, unapoenenda kwa imani, kwa Yasiyoonekana. Ninaona Kanisa likienda katika Unyakuo, ninamwona Yesu akimjia Bibi-arusi Wake, ninaona kundi dogo la watu waliopuuzwa, ambao wanachekwa, na kudhihakiwa, wakiingia katika Unyakuo, siku moja. Ni afadhali niwe pamoja nao kuliko makundi yote ninayoyajua ulimwenguni kote, kwa maana kwa imani tunaona, kwa Yasiyoonekana. Hakika.

⁵⁴ Musa alichagua kuwa...Aliona kwa imani kile walichokuwa, na kwamba Mungu alikuwa ameahidi, katika miaka mia nne, angewakomboa. Hata hivyo, Yeye alikawia kwa miaka mingine ishirini, hata hivyo Musa alimwamini.

⁵⁵ Na sababu ya mimi kuwa hudumani, leo hii, katika mwenendo huu, ni kwa sababu, kwamba, kwa imani. Usiku mmoja, kwenye Kinu cha Green, Indiana, yapata miaka kumi iliyopita, Malaika wa Bwana, ambaye alisema nami tangu utotoni, alisema nami juu ya mambo haya. Nami nikatoka na kujiunganisha. Mara nyingi nisingeamini mambo wanayofanya, lakini hata hivyo, ninaamini, hilo hapo Kanisa la Mungu aliye hai. Na ni afadhali nitembe peke yangu, pamoja na watu wachache ambao kweli wanamwamini Mungu kweli na kuliadini Neno Lake, kuliko kuwa pamoja na mamilioni wanaomkana. Bila shaka! Kazi zao zingefanya hivyo.

⁵⁶ “Musa alistahimili, kama amwonaye Yeye asiyeonekana.” Na mwisho wa safari ya maisha yake. . . Loo, ninapenda tu kusema hivi!

⁵⁷ Mtu fulani wakati mmoja aliniambia, akasema, “Bw. Branham, unafikiri Mungu alikuwa mwenye haki, alipomwacha Musa kwa miaka arobaini pamoja na watu hao, na kisha kumkataza kwenda katika nchi ya ahadi?” Lakini sehemu tukufu ya hadithi ya Musa, alikuwa katika nchi ya ahadi, miaka mia nane baadaye, pamoja na Yesu na Eliya, na alionekana kwenye Mlima Karmeli.

⁵⁸ Si hayo tu, bali hata mwisho wa safari, alipokuwa amesimama juu ya mlima, akiwaaga watu wake kwa

kuwapungia mkono, naye alikuwa ameangalia ng'ambo ya Yordani, naye alikuwa na umri wa miaka mia moja na ishirini, wakati pumzi yake ya mwisho ilipoanza kumwishia, alipanda juu ya ule mwamba uliopigwa kutoka nyikani, na ulikuwepo, wala hakuninii. . . . Alikuwa na Malaika wabebaji waliompeleka mahali fulani na kumzika, hata ulimwengu haukujua lolote juu yake. Kwa sababu, "Alistahimili, akimwona Asiyeonekana." Na katika saa ya kufa kwake, Asiyeonekana alikuwepo. Nashangaa, kama angekuwa farao, kama ingelikuwa hivyo. Nina shaka sana. Lakini alikuwa na uhakika alipochukua chaguo sahihi.

Nawe unaweza kuwa na uhakika, kwa kuchukua chaguo sahihi.

⁵⁹ Yoshua, miaka arobaini baadaye, akiisha kuingia katika nchi ya ahadi, na . . . akiwa jenerali mkuu wa kijeshi. Wakati vita vyake vya kwanza, maadui zake walikuwa wamemzingira mahali ambapo hapakuwa na njia ya yeye kuwafikia. Lakini kwa imani aliangalia Yasiyoonekana, kwa sababu Mungu alimpa Musa ahadi walipokuwa wangali Misri. "Nimewapa Palestina yote." Na kwa imani akaona kuta za Yeriko zimeleleka chini sakafuni. Naye akazunguka na kuzunguka, amevaa silaha kamili, pasipo na shaka lolote moyoni mwake, bali akiamini ya kwamba Mungu angefanya jambo hilo. Ndipo baragumu ilipolia, nao watu wakapiga kelele, kuta zilianguka nao wakauteka huo mji. Kwa nini? Alimwona Yule asiyeonekana.

⁶⁰ Kumbukeni, kabla hajafanya hivi, alikuwa akitembea alasiri moja, naye akamwona Mtu aliyekuwa amesimama kando ya ukuta, amechomoa upanga Wake. Ndipo Yoshua akauchomoa upanga wake, akaenda kumkabili. Naye akasema, "Je, wewe uko upande wetu? Wewe ni wa adui?"

⁶¹ Ndipo yule mtu akajibu na kusema, "Mimi ni Amiri Jeshi wa Jeshi la Bwana." Yoshua alijua ameshinda vita basi.

⁶² Na wakati ninyi watu, hapa, usiku wa leo, ambao ni wenye dhambi mioyoni mwenu. . . . Simaanishi kwamba mnaishi katika uzinzi. Simaanishi kwamba mnalewa. Namaanisha, *dhambi* ni "kutoamini." Na kwa kutokuamini moyoni mwako, kama utaufungua tu moyo wako na kufunga macho yako, na kumwanguka Amiri Jeshi Mkuu ambaye yuko kila mahali usiku wa leo, ulimwengu utalala chini miguuni pako, nawe utatikisa kila pingu za dhambi kutoka kwako. Siku za mashaka zitakwisha. Loo, Jina la Bwana libarikiwe!

⁶³ Naambiwa kuwa nyoka anaweza kushika jicho la ndege, na kumvutia ndege huyo, kwa uganga wake, na kumkazia macho yake, mpaka, hivi kwamba, ikiwa ndege huyo atamtazama huyo nyoka kwa dakika chache tu, ndege huyo atapatatika na kupooza kabisa. Naye huyo nyoka atamchukua huyo ndege.

⁶⁴ Nami naweza kuamini hilo, kwa sababu ninamjua nyoka mwingine, ibilisi, ambaye kama anaweza kuvutia hilo jicho, kwa

uchawi wake, pamoja na muziki wako mamboleo wa roki, na upuuzi wako wote wa ulimwengu. Iwapo anaweza kukushika, ewe msichana ama kijana mwanamume, kwa muda mrefu kutosha tu kukuingizia uloji wake, utapapatika lakini huwezi kujiondoa. Atakushikilia mpaka akumeze katika dhambi.

⁶⁵ Njia pekee, ninaambiwa, ambayo maskini huyo ndege ana nafasi, ni kuyaondoa macho yake kwa huyo nyoka. Na hawezi kutazama kitu kingine chochote, kwa sababu amesimama, akitazama. Lakini kama atayaondoa macho yake kwa huyo nyoka, na kuangalia juu na kupigapiga mbawa zake, ataruka moja kwa moja mbali na huyo nyoka.

⁶⁶ Na kama umewahi kufanyiwa uchawi wa ulimwengu na mambo ya ulimwengu na kutokuamini kukivutia moyoni mwako, kunakokwambia, “Loo, ishi kisasa,” tikisa kichwa chako, usiku wa leo, na kumwalia Yeye Asiyonekana, Bwana Yesu, na upigepige mbawa zako za maombi mpaka uruke moja kwa moja mbali naye na mbali na makucha yake.

⁶⁷ Endapo atasema nawe, na kusema ninii...kwamba, “Uponyaji wa Kiungu ni wa uwongo,” ondoa kichwa chako kwake, upesi. Endapo atakwambia, kwamba, “Upambanuzi wa kiroho ni telepathia,” ondoa kichwa chako kwake, mara moja, na kuangalia kwenye Yasiyoonekana.

⁶⁸ Kama vile Elisha alivyomwambia Gehazi, mtumishi wake huko Dothani. Wakati akiangalia pande zote, kulikuwa na jeshi la Washami. Kulikuwa na kila kitu cha kuwaponda-ponda, kwa sababu mtu huyu wa Mungu aliweza kumwambia mfalme wa Israeli yale mfalme wa Shamu alikuwa akiwazia kwenye chumba chake cha kulala.

⁶⁹ Hebu niseme hivi usiku wa leo, kusanyiko langu. Kwamba Mungu angali hai, Naye ni yeye yule tu usiku wa leo kama alivyokuwa wakati huo. Bado anaweza kujua mawazo yako na yale unayowazia sasa hivi. Ndipo inakupasa kuangalia matunda ya Roho, kuona kama ni Mungu wa historia ambaye amefufuka tena. Bila shaka.

⁷⁰ Ndipo wakati ule msiba mkuu utakapokuja; ambao daima huja. Ndipo wakati Gehazi, akiwa tu mshiriki vuguvugu wa kanisa, wakati... Hakuwa ameona kile Eliya alikuwa ameona.

⁷¹ Kwa sababu, Eliya alizoea kutembea kwa imani, naye alikuwa akiangalia Yasiyoonekana, wakati wote. Naye alijua ya kwamba Mungu alikuwa amesema, katika Zaburi, “Malaika wa Mungu wanafanya kituo kuwazunguka wamchao.” Hilo lilitosha kwa Eliya.

⁷² Lakini Gehazi alikuwa ameta-... ameliadini nusu. Alikuwa tu ni mshiriki wa kanisa.

⁷³ Basi, Elisha akamwambia Bwana, akasema, “Bwana Mungu, tupe ishara hapa. Mfumbue macho mtu huyu na umjalie kuona kile kilichomzunguka.”

⁷⁴ Basi Mungu alipoyafumbua macho yake, aliona farasi wa Moto, wakikokota magari ya Moto, nayo yalimzunguka maskini nabii huyo. Walikuwepo wakati wote, lakini yeye kamwe hakuwaona.

⁷⁵ Na usiku wa leo ningesema jambo lile lile, ya kwamba, Mungu Yule aliyesimama kule katika mlango wa kwanza wa Vitabu vya Matendo; na alipoinuliwa, na mbingu zikawa chini ya miguu Yake. Yesu yuyo huyo alisema, “Tazama, mimi niko pamoja nanyi sikuzote. Sitawaacha kamwe wala sitawapungukia. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya sikuzote. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.”

⁷⁶ Ninaambiwa na marubani wa ndege wanaoendesha hizi hapa, ndege ziendazo kasi sana. Nao wanasema kwamba ndege, inapofikia spidi fulani, kwamba inatetemeka na kutikisika, na inaonekana kana kwamba bolti zitang’oka, kwamba mbawa zitachomoka, mpaka wavuke kizuizi cha sauti. Lakini baada ya kuvuka kizuizi hicho cha sauti, wanasema ndege husafiri tu, kwa urahisi tu, ikivuka kizuizi cha sauti. Hicho ndicho kikwazo kilichoko kwenye njia ya ndege, wakati inapovuka sauti yake yenyewe, kisha inaenda kwa urahisi.

⁷⁷ Loo, laiti Kanisa la siku hizi lingeweza kuomba mpaka wavuke kizuizi cha dhambi, na kizuizi cha kutokuamini, wangeweza kupiga makelele ya ushindi wa Mungu aliye hai, wakiisha kuvuka kizuizi hicho; kwa kuangalia Yasiyoonekana, na kuuacha ulimwengu utetemeka na kufanya utakacho. Lakini kuna Mungu aliye hai. Na tunapopoteza kukosa kwetu imani na kutokumwamini Yeye, na kuvuka mahali hapo ambapo ulimwengu unasema, “Siku za miujiza zimepita,” inakufanya kutikisika. “Loo, hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu,” inakufanya ushanga.

⁷⁸ Lakini kama utaangalia tu Yasiyoonekana, kwa Mungu Yule aliyeyaahidi, “Kwa maana ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na wote watakoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Iwapo utaangalia Neno lililobarikiwa linalosema, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” geuzeni vichwa vyenu na kuendelea mbele, mpaka mpite mtetemo huo, mpite vizuizi vya kutokuamini, na vizuizi vya dhambi, na vizuizi vyote vinavyoonekana kuwazuia. Ndipo mtaruka huru katika imani ya Mungu, mkijua kwamba mambo yote yanawezekana. Ndipo hakuna kikomo, wanasema, angalau, kwa kasi itakayoenda ndege hiyo. Iwapo hakuna kikomo kwa spidi itakayoenda ndege hiyo, hakuna mipaka kwa baraka ambazo Mungu atamwaga juu ya mwaminio atakayeamini.

Maandiko yanamdai kuwa ni “yeye yule jana, leo, na hata milele.”

⁷⁹ Yesu alisema, alipokuwa hapa duniani, “Sifanyi lolote isipokuwa Baba Yangu anionyeshe kwanza.”

⁸⁰ Wakati yule mwanamke kisimani alipomjia, naye alikuwa Msamaria. Kwanza, kulikuwa na mtu aliyemjia, na jina lake aliitwa Petro. Naye akamwambia mtu huyu, “Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona.” Alijuaje jambo hilo? Je, seremala huyu duni wa Nazareti alijuaje kwamba jina la mtu huyo lilikuwa Simoni, na jina la baba yake lilikuwa Yona? Kwa sababu alivikwa Nguvu zinazoweza kuangalia Yasiyoonekana. Kamwe hakuangalia barua zozote zilizoandikwa. Aliangalia Yasiyoonekana, Mungu wa Mbinguni.

⁸¹ Haraka, wakaenda na kumchukua mtu mwingine, nyuma ya mlima, ambaye alikuwa ametoka maili nyingi. Naye alipokwisha kumwambia njiani, yale Yesu aliyokuwa amefanya, bila shaka Nathanaeli alishuku hayo sana. Lakini mara alipofika mbele za Yesu, Yesu alimwambia, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

⁸² Mtu huyu alifanyaje jambo hilo? Hapakuwapo na mtu pamoja Naye wa kusema, “Jamaa huyu ni Mwisraeli.” Alifanyaje hilo? Hakuisoma kutoka kwa kitabu chochote. Bali Yeye aliangalia Yasiyoonekana, kwa Mungu ajuaye mwisho tangu mwanzo.

⁸³ Naye akasema, “Rabi, ulinijua lini?” akasema Nathanaeli.

⁸⁴ Akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Alikuwa akifanya nini? Akiangalia Yasiyoonekana.

⁸⁵ Wakati yule mwanamke kisimani, yule Msamaria, alipotoka, Naye akasema, “Nipe maji ninywe.”

⁸⁶ Naye mwanamke akasema, “Kisima ni kirefu, na huna chochote cha kuchotea.”

⁸⁷ Alisema, “Lakini kama ulijua ni Nani uliyekuwa ukisema naye, ungeniomba Mimi maji unywe.”

⁸⁸ Naye alitaka kujua ni nani aliyekuwa akiongea naye. Naye alijua Yeye alikuwa Myahudi, Naye... Kasema, “Si desturi kwenu Wayahudi kutuomba sisi wanawake wa Samaria kitu kama hicho.”

⁸⁹ Na kwa hiyo mazungumzo yakaendelea mpaka Yesu akashika roho yake. Naye akasema, “Nenda kamwite mume wako, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

⁹⁰ Naye akasema, “Hiyo ni kweli. Una waume watano. Naye yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

⁹¹ Naye akasema, “Tunajua ya kwamba Masihi atakapokuja, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

⁹² Naye akakimbilia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia mambo niliyotenda. Je, haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

⁹³ Na wakati Yesu, katika kuondoka ulimwenguni, baada ya huduma hiyo kote ulimwenguni, kuzunguka ulimwengu unaojulikana wa siku hizo, alisema, “Kazi nizifanyazo ninyi nanyi mtazifanya.” Sikilizeni kuondoka Kwake. “Tazama, kitambo kidogo, na ulimwengu (unaonekana, wa kiakili, wa kitamaduni, wa kisayansi), ulimwengu hautaniona tena.” Huo ni unabii haswa. Hauna lingine ila Kweli. Yesu Kristo alisema hivyo. “Mwaminio wa kiakili, ulimwengu, hautaniona tena. Lakini ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Na kazi nilizozifanya ninyi nanyi mtazifanya. Na zaidi ya hizi mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.”

⁹⁴ Mungu huyu mkuu na Baba tunayezungumza habari zake, si kitu ambacho kilikuwapo. Yeye ni kitu ambacho kipo. Na endapo watu Wake, walioitwa kwa Jina Lake, watavuka kizuizi hicho cha yale ambayo ulimwengu unayo kusema, yale ambayo kanisa linayo kusema, yale ambayo sayansi inayo kusema, na kuangalia yale Mungu anayo kusema; dakika hiyo, utavuka mtetemo huo wa kutokuamini na uwe huru, ukitoka kwenye jengo hili, usiku wa leo, kwa furaha tu uwezavyo kuwa; ukimtumikia Mungu, ukijisikia huru, dhambi zote zimetoweka, umeponywa ugonjwa wako. Mbona, itakuwa ajabu! Mungu asingekuwa Mungu wa haki, ambaye angemzawadia mtu mmoja kwa imani yao, na kutokumzawadia mwingine. Hawezi kulifanya. Kama Mungu aliondoa lukemia kutoka kwa msichana huyo alipokuwa amelala kule; na mojawapo ya hospitali bora sana, Johns Hopkins, ambayo ingeweza kupatikana; na viungo vyake vikianguka kutoka kwake. Na saa moja baada ya maombi kufanywa hapa, mtoto huyo alitangazwa “mzima na mwenye afya,” na madaktari hao hao.

⁹⁵ Mungu hawezi kuwa mwenye haki, kumwacha Mbunge Upshaw, ambaye alikuwa kwenye kiti cha magurudumu kwa miaka sitini na sita, amevunjika mgongo, akitembea kama Bw. Roosevelt, na angemponya mtu huyo na kumtoa kwenye kiti hicho, kwa ono, na kama mtu mwingine akiketi vivyo hivyo, na akawa na imani iyo hiyo, Mungu angekuwa mdhalimu kumponya mmoja na kumwacha mwingine. Yeye ni mwenye haki.

⁹⁶ Ni sisi, marafiki. Laiti tungaliweza kuvuka kizuizi hicho cha sauti! Laiti tungaliweza kufikia mahali ambapo haileti tofauti yoyote ni nani anayesema! Maadamu Mungu alisema ni Kweli, endelea na safari.

⁹⁷ Daima nimefikiria juu ya shairi hilo dogo katika kitabu changu cha shule, nilipokuwa mvulana mdogo hapa barabarani. Wengi wenu wanaume na wanawake wa rika yangu mnalikumbuka. *“Endelea na safari! Endelea na kuendelea na safari!”*

⁹⁸ Wakati Christopher Columbus alipopewa meli na malkia wa Uhispania, na ilikuwa...kwa sababu, moyoni mwake, aliona ono kwamba dunia ilikuwa duara. Naye hakuwa na njia angeweza kulithibitisha. Hakuwa na jambo la kulithibitisha nalo, bali alikuwa mtu wa maono. Aliamini.

⁹⁹ Ndipo alipopewa hiyo meli, pamoja na kundi la wafungwa, waoga; hao walikuwa ni wafuasi wa kanisa lake, kundi la wavuta-nyuma, kundi lililovunjika moyo na kujaribu kumvunja moyo. *“Bado kitambo kidogo na tutaondoka ulimwenguni. Nyoka atainuka kutoka chini ya bahari, na kuzifunga meli hizi ndogo na kuzizamisha. Sasa sema, haramia jasiri, sema! Utasema nini?”*

Akasema, *“Endelea na safari! Endelea na safari! Endelea na uendelee na safari!”*

¹⁰⁰ Mungu, tupe watu Kanisani, namna hiyo. Sijali ulimwengu wa kisayansi unasema nini. Sijali ulimwengu wa kimadhehebu unasema nini. Ninaamini Neno la Mungu, na kuendelea na safari. Endelea na safari, mpaka uvuke kile kizuizi. Tulikuwa, katika kanisa la kale hapa, tulizoea kuimba wimbo huu mdogo hivi:

Nimevuka mstari wa kutenganisha,
Nimeuacha ulimwengu nyuma.

¹⁰¹ Kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo Kanisa linahitaji kuvuka mstari huo ambao unawatenganisha kati ya imani na kutokuamini, kwa kuona, na kuyaangalia Yasiyoonekana kwa imani, ni sasa. Hapo ndipo unapoacha kila kitu nyuma yako, kila wasiwasi, kila uchovu, kila kitu kinachosema kuwa huwezi kuwa Mkristo, *“Nimevuta sigara kwa muda mrefu mno. Nimekunywa pombe muda mrefu sana. Ndugu Branham, nimeishi katika uzinzi.”* Sijali unachosema na kile umefanya, ingawa dhambi zako ni nyekundu sana; wakati mmoja unapita mstari huo wa kizuizi, cha ibilisi akijaribu kukutesa, akisema huwezi kufanya hivyo, huwezi kufanya hivyo. Sema, *“Ninaweza, kwa maana Yesu alisema, ‘Yeyote atakaye, na aje anywe maji ya chemchemi ya Uzima, bure.’”* Yaache nyuma.

¹⁰² Wakati ninyi watu ambao ni wagonjwa, mmepitia mstari wa maombi baada ya mstari wa maombi, na mmeombewa, mmeenda kwa madaktari, mmeifanya kila kitu, na bado kifo kinakaa mlangoni penu. Unapofikia mahali unaposema, *“Sijali daktari anasema nini. Sijali ulimwengu wa kisayansi unasema nini, Yesu Kristo alinitolea ahadi.”* Vuka kizuizi hicho cha mitetemo nafsini mwako, kwamba uko huru. Hakuna kitu kimoja cha

kukutikisa. Utaingia kwenye oponyaji wako hakika tu kama vile ninavyosimama kwenye mimbara hii. Hutawahi kugeuka na kuangalia huko tena. Utakuwa ukiangalia *hivi*.

¹⁰³ Uko huru sana kutokana na vitu hivi: Unasema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama oponyaji wa Kiungu. Huwezi kupona. Ugonjwa wako ni mbaya sana.” Endelea na safari, panda juu yake. Panda zile kuta huko, mpaka kila kitu kiko huru, kila kamba na kila pingu zimekatwa, kila mtikisiko umebaki nyuma, nawe uko huru, na huru kabisa.

¹⁰⁴ Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliketi Kanisani, kwa ajili ya nyinyi watu, kwa ajili ya mambo kama haya. Kwanza aliweka mitume, kisha, baada ya hayo, akatuma manabii, halafu walimu, na wachungaji, na wainjilisti, kuthibitisha Neno hili, kuthibitisha ya kwamba Yeye ni mwalimu fulani mkuu. Simaanishi kuwa lazima awe na Ph.D. Anaweza kujua kidogo kuhusu Biblia kuliko—kuliko mtoto ambaye bado yuko katika ujana wake. Yesu alijua zaidi kuhusu Maandiko, akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, kuliko Mafarisayo wote walivyojua, ama wale wenye hekima wa kale waliosoma. Kwa hiyo, unaona, haihitaji nia ya kiakili. Inahitaji moyo uliojisalimisha kwa mapenzi ya Mungu.

¹⁰⁵ Ikiwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliahidi, Biblia hii, kwamba, “Angeokoa hata wa mwisho.” Ikiwa aliahidi, “Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya. Nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari.” Na kama Yesu yeye yule angeweza kuja usiku wa leo, na kutuchukua katika udhibiti Wake, na tunaweza kujizuia kutowazia jinsi itakavyofanywa, bali kuangalia Yasiyoonekana, kwa Mungu aliyeahidi hilo. “Jambo lile lile nililomfanyia yule mwanamke kisimani, ninaweza kufanya pamoja nanyi. Ishara ile ile niliyounyesha ulimwengu, kwa Myahudi na Msamaria pia, nitaionyesha tena katika siku za Mataifa.” Kama Yeye aliwafanyia hilo, na kujithibitisha Mwenyewe kuwa Masihi namna hiyo, na angefanya lingine lolote na kutuacha tuingie juu ya mambo ya kiakili, haingekuwa haki. Asingekuwa Mungu mwenye haki. Hana budi kuonyesha ishara ile ile. Kama angekuja usiku wa leo, na kutetemeka katika jengo hili na kujionyesha Mwenyewe, ya kwamba yu hai, kwa kufanya ishara zile zile, inapaswa kuufanya moyo wa kila mwenye dhambi kuyeyuka ndani yake. Inapaswa kumfanya kila mgonjwa kusimama kwa miguu yake na kumpa utukufu, na kuvuka kila mstari wa mtetemo, na kuendelea kwenye njia hizo ambapo Mungu anaweza kukuponya na kukupa afya.

Wazieni mambo hayo tunapomba.

¹⁰⁶ Mungu wa rehema na wa Milele, ambaye ulikuwa Mungu kabla ya kuwepo kwa atomi hewani, na utakuwa Mungu wakati hakuna atomi nyingine. Wewe uliyeuumba ulimwengu na kuupima kwa mikono Yako, na kuumwaga angani, na kusema,

“Iwe nuru,” ikawa nuru. Maneno Yako hayawezi kushindwa, wala hayawezi kushindwa usiku wa leo, kwa maana Wewe umetoa ahadi. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Neno hilo ni kweli. Bwana Mungu, tunajua ya kwamba uponyaji umekuwa kitu ambacho kilinunuliwa pale Kalvari, kama tu vile wokovu ulivyonunuliwa. Nasi inatupasa kutazama na kuishi, na kuamini, na kuvuka vizuizi, kukuthibitishia ya kwamba sisi ni waaminifu. Mungu Mwenyezi, tujalie, usiku wa leo, ili watu waweze kuamini, na kuokolewa kutoka katika dhambi zao na magonjwa yao. Nami ningeomba kwamba ungefanya hivi kwa utukufu wa Mungu.

¹⁰⁷ Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, nashangaa tu, usiku wa leo, ni wangapi walio ndani na nje, wangependa kufanya maungamo haya kwa Mungu. “Bwana, ni—nimekuwa mshiriki wa kanisa kwa muda mrefu, au labda sijawa. Lakini, kwa kweli, kuna mengi ya mitetemo ya ulimwengu kwangu. Nina hasira. Nina, loo, kitu ambacho hakitaniruhusu kufikia mahali ambapo ninaweza kuamini kama inavyonipasa kuamini. Je, utaniondolea hilo, usiku wa leo, Bwana? Na jalia nivuke kizuizi cha dhambi cha kutokuamini.” Mtamwinulia mikono yenu? Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Loo, mikono mingi, pande zote.

¹⁰⁸ Bwana, unaona mikono yao. Na naomba Roho Mtakatifu, ambaye sasa amewaambia wainue mikono yao, na aje na kuwaweka huru kutokana na mitikisiko ya dunia, hata waweze kwenda mbali na—na mvuto wa kupooza wa nyoka, hata kuumwa kwa nyoka kwa dhambi, uchawi wa ulimwengu huu wa kisasa hautawavutia tena. Jalia wainue macho yao kwa Kristo sasa hivi na kumpokea kama Mwokozi wao, nasi tutakusifu. Katika Jina la Yesu tunaomba.

¹⁰⁹ Na sasa, kabla hatujawaita wagonjwa na wanaoteseka, kuna wengine humu ndani usiku wa leo, ambao ni wagonjwa, wanaoteseka kwa njia yoyote, ambao wangesema, “Ee Mungu, nijalie nivuke mstari wa kizuizi, pia. Nipe imani ya kuendelea tu kupita mawazo yote ya ibilisi yanayosema, ‘Hutafaulu. Huwezi kuipata’”? Je, mnaweza kuinua mikono yenu, na kusema, “Mungu, unirehemu.” Mungu awabariki. Anaiona mikono yenu yote. Wako kote humu jengoni.

¹¹⁰ Sasa, Baba, jalia kwamba jambo fulani litatendeka, usiku wa leo, litakalowafanya watu hawa kuona ya kwamba hii ni Kweli, Neno la Mungu, na ya kwamba utatimiza ahadi Yako kwao, kama vile tu ulivyomfanyia Ibrahimu, au Musa, au yeyote. Jinsi ambavyo, wakati ulipomwambia Petro, “Tembea uje Kwangu, juu ya maji.” Wala hakuinama kuona ni daraja la aina gani lililokuwa chini ya maji. Hata hakuangalia hilo. Alimtazama Yesu. Lakini alipoelekeza macho yake kwenye mawimbi, angezama. Mungu, tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba wale wanaotoka nje, usiku wa leo, watapita kizuizi hicho cha mawimbi, nao watakwenda moja kwa moja kwa Yesu,

kwa mwaliko Wake wa kuja. Utusikie, Bwana. Na sasa mpe mtumishi Wako hekima ajue la kufanya saa hii, ambayo italeta baraka, wokovu wa uponyaji, wa kimwili na kiroho pia, katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

Asanteni.

¹¹¹ Sasa kwenu ninyi mlioinua mikono yenu. Nitawaombeni jambo fulani. Nitabadilisha ibada kidogo tu, usiku wa leo. Jana usiku tuliwapeleka chumbani. Usiku wa leo, tutajaribu kuwaweka kwenye mstari, na kuleta kadhaa jukwaani. Ndipo, mara baada ya ibada hii kwisha, wakati mchungaji atakapochukua ibada, nitawaomba, ninyi mlioinua mkono wenu, yapata watu ishirini au thelathini, nataka mje na kupiga magoti kwenye madhabahu hii, ikiwa kweli ulimaanisha ulipoinua mkono wako. Unaona, Mungu atalifanya, kama kweli ulikusudia, na utanena tu na kusema, “Bwana, niondolee kila mtetemo wa kutokuamini.” Atafanya hivyo.

¹¹² Unaona, huwezi kwenda huru. Huwezi kufanya hivyo katika ulimwengu wa kisayansi, kwa ndege. Huwezi kufanya hivyo katika ulimwengu wa kiroho, kwa roho, maadamu mawazo yako ya kibinadamu na mawazo ya kiakili, ninayozungumzia, yangali yanakushikilia. “Mbona, . . . makanisa haya hayaamini Hilo. Kanisa hili . . .” Hayafikiri hivyo. Yesu Ndiye aliyesema hivyo. Na kanisa ambalo linakwambia kwamba, “Ni uwongo,” ni unabii wa uwongo. Sisemi hivyo kuwa katili, lakini nasema hivyo kuwa mwaminifu, kwa sababu itabidi nisimame pamoja nanyi kwenye Hukumu. Wale waalimu, wanaofundisha mambo hayo, wamekosea. Sasa hebu . . .

¹¹³ Niwaonyeshe tu kile Yesu alisema, ndipo tutaona jambo kuu, kama linaweza kufanyika. Nadhani kuna watu mia mbili hapa wa kuombewa. Ninataka kuwaombeni jambo fulani, juu ya ujumbe huu sasa, wa *Kuangalia Yasiyoonekana*. Ikiwa Yule asiyeonekana atajitangaza Mwenyewe anaonekana, basi inapaswa kuifanya nafsi yako kupita kila kizuizi. Kama Yeye Asiyeonekana, atajifanya aonekane kwenu, kwa maana Yeye aliahidi angelifanya hivyo. Sasa kumbukeni, katika . . .

¹¹⁴ Sisi ni Mataifa. Sasa, alipokuwa duniani, hapakuwa na mtu yeyote aliyemtafuta ila Wayahudi na Wasamaria. Sisi, Mataifa wa Anglo-Sakson, tulikuwa bado makafiri. Tulikuwa tunaabudu sanamu; baba zetu. Lakini Wayahudi walikuwa wakimtafuta, na Wasamaria walikuwa wakimtafuta. Naye akaja na kuthibitisha ya kwamba Yeye Ndiye waliyekuwa wakimtafuta, nao hawakumwamini. Lakini kulikuwa na baadhi ya wateule waliomjua na kumtambua; Myahudi na Msamaria pia. Sasa itakuwa vivyo hivyo na Mmataifa. Sasa, jinsi alivyojitambulisha kwa Myahudi na Mmataifa, ya kwamba alikuwa . . .

115 Sasa, walisema, “Mnataka—mnataka kumwua kwa sababu gani?”

Akasema, “Kwa sababu Yeye ni Mwanadamu, akijifanya Mwenyewe Mungu.”

116 Alikuwa Mungu na mwanadamu pia. Mungu alikuwa yule mtu wa ndani. Yesu alikuwa mtu wa nje. Wa nje... Yesu alisema, “Sifanyi lolote kwa nafsi Yangu ila lile ninalomwona Baba Yangu akilitenda.” Mtu yeyote anajua hilo. “Kile Baba anachonionesha Mimi, ndicho ninachofanya.”

117 Sasa angalieni jinsi alivyojitangaza Mwenyewe kwa Wayahudi; kwa kumwambia Petro yeye alikuwa ni nani, kwa kumwambia Nathanaeli yeye alikuwa ni nani na kile alichofanya kabla hajaja. Ndivyo hivyo. Nao wakasema, “Wewe...” Nathanaeli akasema, aliposikia hayo, akasema, “Wewe ndiwe Kristo, mfalme wa Israeli.”

118 Lakini Myahudi asiyeamini alisema, ulimwengu wa kanisa, ulisema, “Yeye ni mwana mizimu. Yeye ni ibilisi. Yeye ni Beelzebuli.”

119 Yesu akasema, “Ukisema hivyo dhidi Yangu, utasamehewa,” kwa sababu walikuwa Wayahudi. “Lakini, la sivyo, katika siku za mwisho, wakati Roho Mtakatifu atakapokuja juu ya Mataifa, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao,” wakati Roho Mtakatifu amekuja kufanya jambo lile lile alilofanya, kwa maana Roho Mtakatifu angemshuhudia Yeye. Kwa hivyo tunajiweka katika hali mbaya.

120 Sasa, je, mnaamini ya kwamba Mungu huyo angali ni Mungu aliye hai? Mnaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho za kipindi cha Mataifa? Na makanisa yanamtazamia kuja? Na mnaamini kuwa anawatayarisha kwa ajili ya Kuja Kwake? Vivuli vya Kuja Kwake vinatupwa juu ya nchi; shida, dhiki, mshangao wa wakati.

121 Na kivuli cha Kuja Kwake kimewekwa juu ya Kanisa Lake. Na mambo haya tunayofanya katika Jina Lake ni kivuli tu cha yale atakayofanya atakapokuja. Tunapomwona mtoto amelala pale, akifa kwa lukemia, akirudishiwa uhai katika dakika tano, hicho ni kivuli cha wakati atakapokuja. Mavumbi yaliyo katika nchi yatainuka katika uzuri wa ujana tena. Hiki ni kivuli tu, bali ni kukufanya ujue ya kwamba Yeye yuaja. Hebu tujiachilie na tuweke kando kila pinga sasa.

122 Na kama atakuja, usiku wa leo, na kufanya mambo yale yale aliyomfanyia yule mwanamke kule Samaria na kwa Myahudi, je, ninyi Mataifa mtamwamini, na kuziacha nafsi zenu ziwe huru? Je, mtafanya hivyo? Mwinulieni mikono yenu, mseme, “Nitafanya.”

123 Sasa tunaelewa vibaya, tunaposema “uponyaji,” tunaposema “wokovu.” Hakuna mwanadamu anayeweza kukuokoa. Sijali anachofanya, hawezi kukuokoa; hawezi kukubatiza vya kutosha majini. Hawezi kufanya chochote kukuokoa. Kristo anakuokoa. Lakini amekutengenezea njia ya kuokolewa. Anaweza kuhubiri Neno, anaweza kubatiza kwa maji, lakini Kristo anabatiza kwa Roho Mtakatifu. Ndivyo alivyosema Yohana, “Mimi ninabatiza kwa maji, lakini Yeye ajaye nyuma yangu hubatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto.” Yesu anaweza kuonyesha ishara Zake za kuwa hapa, akihubiri Neno Lake kwa mhudumu, na kushuka na kulithibitisha Neno hilo kwa Yeye kuwa hapa; bali unaponywa kwa imani yako. Unaona?

124 Sasa na tuwe na kicho tu kadri tuwezavyo kuwa; na, tafadhalini, sasa, tafadhali. Sisemi kwamba atafanya. Lakini tutaitisha mstari mdogo wa maombi hapa. Na kuna kundi hapa ndani, nadhani, kama sijakosea, waliniambia walikuwa wamesambaza kadi mia moja. Hiyo ina maana kwamba kuna watu mia moja wanaoketi hapa wa kuombewa. Tutawafikia, kila mmoja. Ikiwa tu hamtavunjika moyo na kutoroka, tutamfikia kila mmoja wenu. Mnaona? Hatuwezi kuwaita wote kwa wakati mmoja, wala hatuwezi kuwasimamisha wote kwa wakati mmoja. Lakini tunaweza kuwasimamisha baadhi yao kwa wakati mmoja, labda wanne, watano, au sita, wowote tunaoweza kuwaleta jukwaani hapa, ama juu na chini kando, ambapo tunaweza kuwasimamisha, kwa sababu hatuna nafasi. Lakini ikiwa Mungu atawafanyia kama alivyofanya, kujithibitisha Mwenyewe ya kwamba yuko hapa, basi yatupasa kuangalia Yasiyoonekana basi na kuamini.

125 Enyi wagonjwa wote mlioinua mikono yenu, kama Yesu atakuja na kufanya jambo lile lile alilofanya alipokuwa hapa duniani, kupitia miili ya wanadamu. . .

126 Nilistaajabu hivi majuzi, nilipomwona mmoja wa walimu wakuu sana, nilivyodhani, ulimwenguni. Ni mtu mkubwa. Msinieleme vibaya. Billy Graham, ambaye Bwana anamtumia, mtu mashuhuri. Lakini ilikuwa ni makala gazetini, ambayo baadhi ya . . . mtu fulani mahali fulani alikuwa amemwandikia, na alitaka kujua, “Vipi kuhusu utatu? Je, kulikuwa na Miungu watatu, halisi, au kulikuwa na Mungu mmoja tu?”

127 Naye Billy Graham akamjibu, na kusema, “Bado haijafunuliwa.” Tunalo gazeti hili.

128 Loo, ndugu, usiamini kamwe kuna Miungu watatu. Kuna Mungu mmoja tu. Kuna ofisi tatu za huyo Mungu mmoja. Ubaba, Uwana, na Roho Mtakatifu; Mungu akijishusha cheo kutoka Mbinguni. Alikaa mlimani, katika Nguzo ya Moto. Alishuka na kufanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, katika Uwana, kutoka kwa Ubaba. Na sasa anakaa katika Kanisa Lake, kama

Roho Mtakatifu. Mungu yeye yule! Si Miungu watatu. Mungu yule yule! Mnaona? Mungu yule yule!

¹²⁹ Sasa, tazama, alipokuwa hapa duniani. Sikiliza kwa makini sasa. Alipokuwa hapa duniani, alisema hivi, “Bado kitambo kidogo, ulimwengu hautaniona, hata hivyo ninyi mtaniona. Ninatoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu.” Ni wangapi wanaojua Maandiko yanasema hivyo? Vema, jinsi alivyokuwa wakati alipokuwa hapa duniani, basi hapana shaka alirudi kufanya jambo lile lile. “Na bado kitambo kidogo, nami nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Mnaona? Hilo linamfanya Yeye yule. Tawi lilo hilo, linaendelea tu kutoka kwenye ule Mzabibu. Mnaona? Mnaona? Tawi moja *hapa*, wakati mwingine wa kanisa *hapa*, mwingine *hapa*; ni matawi kutoka kwa ule Mzabibu. Sasa mwangalieni Yeye katika tawi pale.

¹³⁰ Alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema alitoka kwa Mungu, ambaye alikuwa ni Nguzo ya Moto, Naye akasema alirudi kwa Mungu.

¹³¹ Baada ya kifo Chake, kuzikwa na kufufuka, Paulo alikuwa akienda zake Dameski, ndipo Kitu fulani kikambwaga chini. Mnakumbuka hilo? Matendo, mlango wa 8, naamini. Naye alipotazama juu, ile Nguzo ya Moto iliyokuwa nyikani, Yesu Kristo alikuwa amegeuka tena kuwa Nguzo ya Nuru iliyoyapofusha macho yake. Je, hiyo ni kweli? Basi alikuwa amerudi kwa Mungu. Naye Paulo akasema . . .

Akasema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.” Alikuwa ni Nguzo ya Moto.

¹³² Ninasema hivi kwa maskani, si kwa kukufuru, bali mnajua Yeye yule, Roho yeye yule, yuko pamoja nasi sasa? Tunayo picha Yake imening’inia hapa, na ulimwengu wa kisayansi. Nazo ishara alizofanya kule nyuma, zinaonyesha ya kwamba Yeye angali anaishi katika Kanisa Lake; si aina nyingine ya ishara, bali ishara ile ile. “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena,” wenye akili, “lakini, ninyi,” ambao mmevuka kizuizi cha sauti, kuliadini Neno, “mtaniona Mimi.” Natumai kuwa uko ndani ya hao “ninyi” usiku wa leo.

Na tuombe.

¹³³ Bwana, sasa, ibada iliyosalia, itabidi iwe ni Wewe, baada ya maneno kama haya, kuthibitisha kwamba umesema Kweli. Ninaomba ya kwamba utatujalia baraka hizi, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹³⁴ Sasa ni wangapi . . . Ninyi mlio na kadi za maombi hapa ndani, hatuwezi kuwasimamisha nyote kwa wakati mmoja. Lakini kama tu hamtavunjika moyo, usiku wa leo, kesho usiku, Jumapili na Jumapili usiku, na kadhalika, tutawafikia. Lakini

sasa hebu tuanze usiku wa leo, na tuanze kuleta wachache tu hapa juu. Na wale ambao wana kadi, ambao hawawezi kutembea, nitawaita mmoja baada ya mwingine na kuwaweka hapa. Ikiwa huwezi kutembea, ninapoita namba yako, basi inua mkono wako, halafu baadhi ya mabawabu hapa watakuja kukuchukua. Vema.

¹³⁵ Kadi ya maombi namba moja, ni nani aliye nayo? Inua mkono wako kama una kadi ya maombi namba moja. Inua mkono wako. Hakika. Mtu fulani labda hawezi. . . Vema, labda nilikosea. Billy yuko wapi? Labda ilikuwa. . . Ati nini? [Mtu fulani anasema, “A moja?”—Mh.] Naam, sawa. Kama unaweza kutembea, bwana, njoo papa hapa.

¹³⁶ Kadi ya maombi namba mbili. Kama unaweza kuinua mikono yako, inua mkono wako. Vema.

¹³⁷ Namba tatu. Papa hapa, naomba uje papa hapa, kama unaweza. Sasa, kama huwezi, endelea tu kupunga mkono wako, na baadhi yao watakuja kukubeba. Namba tatu.

¹³⁸ Namba nne. Herufi gani hiyo? [Ndugu mmoja anasema, “J.”—Mh.] J? Vema. Namba nne, tafadhali inua mkono wako. Huyu mama huko nyuma, tayari amesimama.

Namba tano.

¹³⁹ Sasa wakati Billy anaposhuka kuzisambaza kadi za maombi, ama Leo, ama Gene, Ndugu Wood, au mtu awaye yote anayezisambaza, wanakuja hapa mbele zenu, na kuchanganya kadi hizo, pamoja, na kukupa kadi yoyote ya maombi unayotaka. Mnaona? Hiyo ni juu yako, chukua tu kadi yako. Unaweza. . . Mtu anayeketi karibu nawe unaweza kuwa na namba moja, anayefuata unaweza kuwa na namba kumi na tano, nyuma hapa awe na nambari mbili. Zinachanganywa tu. Vema.

¹⁴⁰ Kadi ya maombi namba tatu, ni nani aliye nayo? [Mtu fulani anasema, “Pale.”—Mh.] Huku? Vema.

Namba nne.

¹⁴¹ Namba tano. [Ndugu mmoja anasema, “Ninayo namba tano.”—Mh.] Namba tano.

¹⁴² Namba sita. Huko nyuma kabisa, vema. Tafadhali, hapo nyuma, mwacheni tu maskini mama huyo apite.

¹⁴³ Namba saba, unaweza kuinua mkono wako. Yako ni namba saba, dada? Vema.

¹⁴⁴ Namba nane, naomba uinue mkono wako, kama unaweza. Huyu mama papa hapa, namba nane. Vema, dada, chukua mahali pako.

Namba tisa. Huyu mama hapa. Sawa, dada.

¹⁴⁵ Namba kumi. [Mtu fulani anasema, “Papa hapa pembeni.”—Mh.] Vema. Namba kumi. Hebu—hebu tuachie hapo, maana tunasongamana huko kidogo. Kama watarudi nyuma kidogo tu,

tafadhalini. Vema, tutaita kumi. Sasa, nadhani . . . Una ya kumi, sivyo, dada? Kama mnaweza kusonga mbele moja kwa moja, hao waungwana papo hapo, watakuruhusu uingie mstarini. Sasa, vema.

¹⁴⁶ Ni wangapi? [Mtu fulani anasema, “Tisa.”—Mh.] Namba tisa haipo. [Ndugu mmoja anasema, “Hapana. Papa *hapa*, Ndugu Billy.”] Loo, pale—pale, hawezi, loo, kama hawezi kutembea, mwacheni tu aketi hapo kisha mumlete namba yake itakapoitwa. Atakuwa sawa. Wakati tu namba yako . . . Kama huwezi kusimama kwa muda mrefu sana, dada, ngojea tu mpaka namba yako iitwe, ndipo unaweza kuja. Hiyo ni sawa. Vema, ke—ketini tu. Hiyo ni sawa. Sasa, kama hawezi kutembea, vema, namba yake itakapoitwa, baadhi yao watambeba wamlete hapa, ama chochote kile. Hiyo ni sawa. Vema.

¹⁴⁷ Namba, ni namba nyingine gani tulikuwa tumeikosa? [Ndugu mmoja anasema, “Hao ni wote.”—Mh.] Ni hao tu. Vema. Sasa tuna wangapi? Je, huo ndio mwisho wa mstari papo hapo? Vema, sawa.

¹⁴⁸ Sasa, ninataka kujua ya kwamba ninyi nyote katika mstari huu, ambao mmesimama kwenye mstari hapa sasa, nataka kuwaulizeni swali hili. Je, mnaamini kwa dhati kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu? Tena mnaamini kwamba amefufuka katika wafu? Naye hajafa sasa, bali Yu hai. Je, mnaamini kwamba—kwamba Yeye anaweza kufanya na kutekeleza yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani? Na mnaamini ya kwamba amemtuma Roho Wake katika Kanisa Lake, kuendeleza kazi Yake?

¹⁴⁹ Ni wangapi wenu hatufahamiani, inua mkono wako? Sikujui wewe. Sawa. Sikujui wewe. Sawa. Sawa. Huo ulikuwa ni kila mkono? Mikono yote ilikuwa juu, kwamba hawanijui? Vema. Sifahamiani na watu hao. Sijawahi kuwaona.

¹⁵⁰ Ni wangapi humu jengoni ambao hatufahamiani, kwamba siwajui ninyi. Hapana, si lazima uwe hapa, popote pale tu. Vema, naona, zaidi ya nusu ya kusanyiko hatufahamiani. Sawa. Kama hatufahamiani nanyi, ninataka kuwaulizeni huko nje kwenye—kwenye kusanyiko. Kama Yesu alikuwa hai leo . . . Na muone kama haya ni Maandiko.

¹⁵¹ Wakati mmoja kulikuwa na mwanamke ambaye alikuwa na tatizo kubwa, kutokwa na damu. Alikuwa nalo kwa yapata miaka kumi na miwili, naamini, ama zaidi. Naye alikuwa ametumia pesa zake zote kwa madaktari.

¹⁵² Hawa hapa wasichana wawili wameketi kwenye viti vya magurudumu. Mnaamini, enyi wasichana, kwamba Yesu amefufuka katika wafu? Mnamtazamia usiku wa leo kwa ajili ya afya? Je, mna—mna ninii yoyote . . . Je, mna kadi ya maombi? Vema. Bado haijaitwa. Hiyo ni sawa. Iweni tu waaminifu. Vema.

153 Usiwe na shaka. Amini tu sasa. Na kama kadi yako haitaitwa usiku wa leo, rudi tu kesho usiku, unaona. Endelea tu... Haidhuru, endelea tu kuja, unaona, itafika hapa. Wala sio lazima hata uwe na kadi yako. Amini tu. Angalia kinachotukia.

154 Na kwenu ninyi huko nje kwenye kusanyiko, ambao hamna kadi ya maombi. Ni watu wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi? Inueni mikono yenu. Angalieni hapo. Sasa ninyi msio na kadi ya maombi, kama watu hawa hapa...

155 Nitayawekea msingi kwenye Maandiko. Kila jambo tunalopaswa kufanya lazima liwe la Kimaandiko, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo. Ni lazima iwe ni Mungu. Kama nilivyozungumza jana usiku, lazima iwe hivyo “tangu mwanzo.” Mnaona? Sasa, kama huna maombi... Hawa hapa ambao wana kadi ya maombi, nitawauliza Maandiko kama ilivyomaanisha katika Biblia, wanaume na wanawake pia.

156 Na kwenu ninyi huko nje, ambao hamna hii, ka—kadi ya maombi, ambao hamtakuwa mstarini, usiku wa leo. Sasa, mnaweza kuwa na kadi za maombi tena kesho. Lakini sasa... Naye atamaliza. Kuna wengi, nasi tutawapitisha hapa, kwa namna fulani, na kuwaombea, kama tu mkivumilia. Msiwe na haraka; mnaona, ndipo mnaanza kujitetemesha wenyewe. Mnaona? Simama tu kimya, useme, “Mungu, niko hapa. Unanijua.” Na—na, basi, unasema hivi.

157 Kuna Maandiko katika Biblia, ambapo mwanamke huyu alikuwa na kutokwa na damu, naye akapitia kwenye kundi la watu waliokuwa wakijaribu kumfanya atulie. Naye alitaka kufika kwa Bwana, Bwana Yesu. Na hatimaye akafika mahali alipokuwa, kwa maana alisema moyoni mwake, “Kama nikiweza kugusa vazi la Mtu huyo, nitapona.” Ni wangapi wamewahi kusikia hadithi hiyo? Sasa, Yesu, akiambatana na umati, na baada ya kitambo kidogo yule mwanamke akamgusa. Moyoni mwake, aliwaza. Alifanya nini basi? Hayo yalikuwa matarajio yake. Alipogusa hilo, alipita kizuizi cha sauti. Hilo ndilo. Alikuwa huru. Maana moyoni mwake, alisema, “Nimefanya kile hasa nilichofikiria. ‘Nikifanya hivyo, ningepona.’”

158 Basi unaamini, kama Yesu atajitambulisha usiku wa leo, utapata jambo lile lile? Vema. Sasa amini tu. Weka hilo moyoni mwako.

159 Ndipo akatoka, akaingia kwenye kusanyiko mahali fulani, labda, na kuketi. Yesu akasimama, na kusema, “Nani aliyenigusa?”

160 Nao wakasema, “Hakuna aliyekugusa.” Kila mtu akasema, “Hatukukugusa. Hatukukugusa.” Kila mtu alikana. “Hakuna aliyekugusa.”

161 Naye Petro akasema, “Bwana,” akamkemea, na kusema, “kwa nini useme jambo kama hilo?” kitu kama hiki, “Ati ni nani aliyekugusa?” wakati kila mtu anakugusa, wanakusukuma?

‘Aloo, Rabi! Nimefurahi kukutana na Wewe, Rabi! Aloo, Yesu, Nabii wa Galilaya! Tu—tuna furaha kukutana Nawe! U hali gani?’ Kila mtu anakugusa.”

¹⁶² Akasema, “Hiyo inaweza kuwa ni kweli. Lakini mtu alinigusa vinginevyo.” Huo ndio mguso unaotaka. “Mtu fulani alinigusa kwa njia ambayo walipita kizuizi cha sauti. Nilihisi nguvu, udhaifu, ukanijia, nguvu zikanitoka.”

¹⁶³ Naye akaangalia pande zote. Na ndani yake alikaa Roho wa Mungu. Mnaamini hilo? Naye akatazama huku na huku, juu ya kusanyiko, mpaka akampata mtu aliyekuwa amemgusa. Naye akamwambia hali yake, na kusema ya kwamba imani yake ilikuwa imemwoko. “Hakuna ono?” Hapana, alijua tu kwamba imani yake ilikuwa imemwoko, kwa sababu mvuto wa imani yote mle ndani, ulikuwa mkubwa zaidi ndani yake.

¹⁶⁴ Sasa, iwapo Yesu ni yeye yule leo, Yeye si atafanya vivyo hivyo? Sasa, utajuaje kuwa ni Yeye? Unaona, sasa, unapaswa kujisalimisha.

Sasa hapa ndipo inabidi niangalie Yasiyoonekana.

Je, wewe ndiye wa kwanza? Iko wapi?

¹⁶⁵ Nani yuko kwenye. . . anayepangisha mstari? Wewe, Ndugu Neville? Loo, Billy. Vema.

¹⁶⁶ Wewe ndiye mtu wa kwanza? Vema. Sasa unaweza tu kupiga hatua chache ukaribie, tafadhali, bwana.

¹⁶⁷ Huyu hapa mwanamume ambaye nime. . . Ninaamini ulisema hatufahamiani, kwa hivyo hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Nitamjuaje mtu huyo? Simjui. Mungu anajua, kadiri—kadiri ni juavyo mimi, sijawahi kumwona maishani mwangu. Huyu hapo mgeni kabisa.

¹⁶⁸ Sasa, nimesema kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, hiyo ni kutumia imani nyingi. Kama sivyo, basi nimepatikana kuwa mnafikiri, na Biblia ni uwongo. Sasa, inanibidi kufanya nini sasa? Kutazamia jambo fulani la kiakili? Ninawezaje? Sina budi kuangalia Yasiyoonekana. Lakini kwa nini ninafanya hivyo? Aliahidi hilo. Haya basi. Sasa, *wewe* fanya vivyo hivyo, na *wewe* ufanye vivyo hivyo. Ninyi nyote fanyeni vivyo hivyo. Haliwezi kushindwa. Ninaweza kushindwa, unaweza kushindwa, lakini Mungu hawezi kushindwa.

¹⁶⁹ Sasa hawa hapa wanaume wawili, wamekutana mara ya kwanza maishani mwao. Sasa, kusudi nichukue wakati wangu.

¹⁷⁰ Sasa, haya ni mandhari ya Kimaandiko. Kulikuwa na mtu aliyekwenda na kumchukua mtu, na kumleta kanisani, ama mahali Yesu alipokuwa, na jina lake aliitwa Nathanaeli. Yesu hakuwa amemwona. Basi alipomjia Yesu, Yesu alisema, “Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.”

¹⁷¹ Ikiwa ningesema hilo ili mjue ninachosema, ningesema, “Yule pale mtu mwaminifu, Mkristo mwaminio.” Wangesema . . .

¹⁷² “Mbona,” akasema, “Rabi, mbona, hujawahi kuniona maishani Mwako. Unanijuaaje? Ulinijuaaje?” Sasa, si jinsi alivyokuwa amevalia, maana Wamashariki wote walivalia vile vile. Angeweza kuwa Mgiriki. Angeweza kuwa Mmisri. A—angeweza kuwa mambo mengi.

¹⁷³ Lakini Yesu alisema, “Yeye ni Mwisraeli. Naye ni mwaminifu, wala hakuna hila ndani yake.”

Akasema, “Ulijuaje jambo hilo?”

¹⁷⁴ Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Huyu alikuwa ni Yesu jana.

¹⁷⁵ Kama ni yeye yule leo, na akiishi ndani yetu, wakati alipoahidi atafanya, na atamjulisha mtu huyu. Huenda yuko hapa kwa shida za kifedha. Huenda ikawa ni mtu anayekufa. Anaweza kuwa mtu wa dhambi. Anaweza kuwa mtu wa haki. Sijui. Siwezi kuwaambia, lakini Mungu anajua. Basi, kama atajidhihirisha Mwenyewe hapa, ya kwamba Yesu yu hai, na atamwambia mtu huyo, basi na awe mwamuzi kama ni kweli au la. Na basi hilo lingewafanya ninyi nyote kumwamini Yeye? kwamba Yeye anaonekana hapa. Huo ni Utu Wake. Sasa, Yeye hawezi kujionyesha Mwenyewe katika mwili wa nyama. Ni Roho Wake.

¹⁷⁶ Sasa, aliruhusu picha Yake ipigwe pale, mnaiona ile, ambayo ulimwengu wa kisayansi unayo huko Washington, DC. Malaika yule yule wa Mungu, Nguzo ile ile ya Moto, aliyeshi ndani ya Yesu, alifanya jambo lile lile kwa—kwa Filipino, au Nathanaeli. Yesu yeye yule aliahidi kuja na kukaa ndani yetu, na kufanya kazi zile zile. Kila mtu anaelewa vizuri sasa? Vema.

¹⁷⁷ Sasa, Bwana, na ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu, na ya kuwa sisi ni watumishi Wako. Halafu, unatupenda. Nawe unataka watu hawa wakuamini, na kuvuka viziuzi vyote vya dhambi ulimwenguni, wapate kuokolewa na kuponywa kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

¹⁷⁸ Sasa, kusema tu kama Petro alivyofanya kwenye lango liitwalo Zuri, kwa mtu aliyekuwa kilema tangu tumboni mwa mamaye, alisema, “Tuangalie sisi.” Hiyo ilikuwa tu ku—kuamini, kumfanya aninii . . . usikivu wake, kuvutia usikivu wake.

¹⁷⁹ Kama vile Bwana wetu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani. Akamshika na kuyashika maongezi yake. Kasema, “Nipe maji ninywe.” Unaona, wakaendelea, wakizunguma.

¹⁸⁰ Sasa, kama sikujui, wewe ni mwanamume tu ambaye alikuwa huko nje kwenye kusanyiko. Na ikiwa sikujui, naye Bwana atanielezea jambo ambalo umefanya maishani mwako, au kile unachotamani, fedha, afya, au chochote kile, na atafanya kweli na wazi, basi utaamini kwamba Yeye yuko hapa kukupa

kile unachoomba. Utafanya hivyo? [Ndugu huyo anasema, “Amina. Hakika nitafanya.”—Mh.] Vema.

¹⁸¹ Kicho sasa. Sasa iweni tu katika maombi, mpaka Roho Mtakatifu atakapoanza kutulia juu yetu.

¹⁸² Naam. Namwona mtu huyu. Naye...Ninamwona mtu mdogo ambaye amesimama karibu, ambaye anahojiwa, au, anataka kuombewa. Ni mtu mwingine unayetaka aombewe. Huyu ni m—msichana, msichana mdogo. Wala hutoki humu nchini. Unatoka karibu na zi—ziwa kubwa, mahali fulani. Ni, unatoka katika mji ambao uko karibu na jiji kubwa ambalo lina kuba kubwa. Ni Buffalo, New York. Uko karibu na Buffalo, New York. Una shinikizo kuu la damu. Hiyo ndiyo shida yako. Lakini unamwomba mtoto huyu. Je, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? [Ndugu huyo anasema, “Kabisa.”—Mh.] Wewe ni Bw. Holden. Hilo ndilo jina lako. Rudi nyuma na upokee ulichoomba. Weka lesa hivo juu yake, utakwisha...? . . .

¹⁸³ Je, unaamini Yesu Kristo yu hai? Ni nini? Yasiyoonekana yanakuwa ya kuonekana. Hiyo ni nini? Yesu yeye yule, matunda yale yale, ishara zile zile, jambo lile lile alilofanya.

¹⁸⁴ Sasa huyu hapa mwanamke, anayefuata. Ninazungumza naye kama Yeye alivyozungumza na yule mwanamke kisimani. Hivi hatufahamiani? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Hatufahamiani. Kusudi watu wajue, huko nje, i—inua tu mkono wako juu. Kwa hivyo huu ndio mkutano wetu wa kwanza. Hatufahamiani.

¹⁸⁵ Sasa, sijui mtu huyu alikuwa na nini dakika chache zilizopita, lakini, chochote kile, sikuhusika na uponyaji wake. Mungu alifanya hivyo. Imani yake ilifanya hivyo. Sikuhusika kwa chochote. Ni karama tu.

¹⁸⁶ Kwa maana, katika jengo hili sasa, ni aina ile ile ya Malaika tu ambao Gehazi aliwaona wakati Elisha alipoyafumbua macho yake. Ndani ya jengo hili yuko Bwana Yesu. Kwa hiyo, usiangalie kile unachokiona. Angalia kile usichokiona. Kwa sababu, ni ahadi ya Mungu ambayo Mungu alisema angefanya jambo hili, na Yeye analifanya.

¹⁸⁷ Sasa, Yeye alizungumza na mwanamke huyo kwa dakika moja tu, mpaka akapata shida yake ilikuwa ni nini. Na hivyo ndivyo ningetaka kuwatendea, kwa maana Yeye hudumu yeye yule. Iwapo hatufahamiani, wala sikujui, basi Yeye ataninii. . . Itabidi iwe kwa njia fulani, ya kimbinguni, kwa njia fulani, kuwasiliana nawe. Je, mng'amini kwamba huyo alikuwa ni Bwana wenu akiniruhusu kufanya hivyo?

¹⁸⁸ Sasa, mkitaka kujua, kulikuwa na jambo fulani lililutukia mle jengoni wakati huo tu, uponyaji. Ni mwanamke aliyeketi hapa, papa hapa kwenye kusanyiko, kwa namna fulani ni mwanamke mnene. Ameinua mikono yake juu, na macho yake yamefumbwa, akiomba. Ana shida ya utumbo na shida ya

mgongo, naye anaomba Mungu amponye. Ameketi papa hapa, amevaa miwani, amevaa suti nyeusi, moja kwa moja mwishoni mwa safu hii.

¹⁸⁹ Wewe ambaye umeinua mikono yako, hiyo ndiyo ilikuwa shida yako. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako namna hiyo. Sikujui wewe, sivyo? Hapana, bwana. Hatufahamiani. Nenda nyumbani sasa. Uligusa upindo wa vazi Lake. Ulingusa Yeye, kwa maana niko futi ishirini kutoka kwako. Lakini ulingusa Yeye, Kuhani Mkuu ambaye angeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.

¹⁹⁰ Sasa, ninyi wengine. Kuna mama asiye na kadi, bila chochote, ameketi tu pale akingojea. Wewe fanya vivyo hivyo. Baadhi. . .

¹⁹¹ Wewe ni mke wa mtu aliyekuwa hapa hivi punde, maana ninawaona nyote wawili katika nyumba moja. Nawe unaugua ugonjwa wa fadhaa. Pia, naona umekuwa kwa daktari na umefanyiwa uchunguzi, na huo uchunguzi ulikuwa wa sehemu za chini. Naye anasema, kwa kuangalia, "Inasema ni uvimbe." Na huo uko kwenye tumbo na katika viungo vya kike, naye anataka ufanyiwe upasuaji, lakini umekuwa na imani, na kuamini kama ungekuja hapa nami ningekuomba, ungeponywa. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako, watu wataona.

¹⁹² Sasa, Yeye ambaye anamjua hapa, na anajua hali ya mambo, je, anaweza kufanya hivyo?

Njoo hapa.

¹⁹³ Bwana Yesu, jalia, Ee Mungu, kwamba imani yake na furaha yake ijazwe, usiku wa leo, kwamba atawekwa huru kabisa, na kuleta furaha na wokovu kwa wale anaowasiliana nao. Nilimtuma. . . na kuutupilia mbali uovu huu kutoka kwake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁹⁴ Unajisikia tofauti sasa. Endelea tu kujisikia hivyo, na kushangilia, utakuacha kabisa, milele.

¹⁹⁵ U hali gani? Iweni tu na kicho kabisa, hebu kidogo tu. Nijuavyo mimi, mara yetu ya kwanza kukutana. Lakini Mungu anatumia sote wawili. Anajua kukuhusu na anajua kunihusu. Na kama atanifunulia kile kilichokuleta hapa, ama jambo ambalo umefanya, ambalo hukupaswa kufanya, au jambo ulilopaswa kufanya, ambalo hukufanya; lakini anajua sina fununu ya kile kilichokuleta hapa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Lakini ingekuwa, itabidi ije kupitia upambanuzi fulani wa kimbinguni. Nina furaha sana kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

¹⁹⁶ Huombi maombi kwa ajili yako mwenyewe, ingawa unayahitaji. Unaomba kwa ajili ya mwanao. Naye mwanao hayupo hapa. Yuko katika jiji kubwa, jiji kubwa, na liko

Mashariki. Nimekuwa huko. Kampeni yangu ya mwisho ilikuwa huko, Filadelfia. Hiyo ni kweli. Yeye ni mhubiri. Nao watamfanyia upasuaji. Nao wanamchunguza kwa ajili ya hena. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Unaamini kwamba Mungu atafanya kile unachomwomba? [Dada huyo anasema, “Ndiyo. Ndiyo, ninaamini. Ndiyo, kweli ninaamini atafanya.”—Mh.]

¹⁹⁷ Ee Mungu wa Milele, thibitisha imani ya mwanamke huyu kwa ishara na ajabu. Mjalie ukombozi wa hiki anachoomba. Kupitia Jina la Yesu Kristo ninaomba. Amina.

Mungu na akupe hicho ulichoomba.

Na mwe na kicho.

¹⁹⁸ Maskini mama aliyeweka lesa yake hadi puani, akiombea maumivu ya kichwa chake. Je, unaamini Bwana Yesu amekuponya? Mwanamke anayeketi papa hapa karibu na huyo mtu aliyevaa miwani. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, maskini mama uliyevaa vazi la rangi ya buluu? Inua mkono wako ikiwa hiyo ndiyo ilikuwa shida. Nenda ukaponywe. Imani yako imekuponya.

¹⁹⁹ Je, unaamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, angeweza kunifunulia kile kilichokuleta hapa? Una shida nyingi; fadhaa kubwa, shida, matatizo ya kike, shida ya kina mama, karibu kurukwa na akili, ugonjwa mbaya sana. Wewe hutoki katika mji huu. Hata hivyo, unatoka Indiana, Lafayette. Bibi Elison, rudi. Ugonjwa wako umekuacha. Nenda nyumbani ukaonyeshe kile ambacho Mungu amekutendea. Amina.

²⁰⁰ Je, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia uko hapa kwa sababu gani? Kama akiniambia, utamwamini kwa moyo wako wote? Huko hapa kwa sababu yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mtoto huyo. Ikiwa Mungu ataniambia shida ya mtoto huyo ni gani, utaniamini? Ni uvimbe wa damu. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini, kama nitamwomba Mungu autoe huo kwa huyo mtoto mchanga, huyo mtoto ataishi?

²⁰¹ Inamisheni vichwa vyenu. Sasa, huyo mtoto ni mdogo sana kuwa na imani. Unaona?

²⁰² Ee Bwana Mungu, walikuletea watoto wadogo, Nawe ukawabariki. Na Yesu yuyo huyo amesimama hapa sasa.

²⁰³ Ninamlaani ibilisi huyu ambaye anajaribu kuchukua maisha ya mtoto huyu mchanga. Mwache, ewe Shetani. Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani ya huyo mtoto mchanga.

²⁰⁴ Sasa mchukue. Usitie shaka. Kitu hicho kitamwacha huyo mtoto. Kuwa na imani.

²⁰⁵ Baba, unayeketi hapo umeinamisha kichwa chako, ukiwa na ugonjwa huo wa kibofu nyongo. Sikujui, lakini Yeye anakujuu. Unaugua mashambulizi ya kibofu nyongo. Na una shinikizo kubwa kifua ni mwako. Ikiwa hiyo ni kweli, pungua mkono wako.

Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Basi nenda nyumbani, kutoka kwenye mkutano huu, na kamwe usiugue huo tena. Uwe mzima, katika Jina la Bwana Yesu.

²⁰⁶ Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Ikiwa Mungu ataniambia shida yako, utaamini kwa moyo wako wote?

²⁰⁷ Sasa, kuna jambo linalotendeka humu jengoni. Endelee ni tu kuamini. Lakini kuna kitu kinachoingia, chenye nguvu, chenye nguvu sana. Kuna mama mweusi amesimama kando ya mama huyu. Inaendelea kufifia tu. Ninamwona mwanamke mweusi. Ameketi papa *hapa* nyuma. Ana yabisi kavu na magonjwa ya ziada. Ameketi moja kwa moja karibu na Bibi Bell pale. Amevaa kofia nyeusi. Simjui. Lakini, dada, kama utamwamini Mungu jinsi ulivyomwahidi wakati ule ungemwamini, itakwisha.

²⁰⁸ Sasa, ili mpate kujua ya kwamba huyu ni Roho wa Mungu. Mstari unaofuata, nyuma ya huyo mwanamke, mwanamume anayeketi hapo na matatizo ya shingo yake. Kama utaamini, bwana, Mungu atakuponya kama utaamini. Je, unaamini? Inua mkono wako. Hatufahamiani na wewe, lakini Yeye anakufahamu.

²⁰⁹ Unaona, popote ulipo, mwamini tu Mungu. Je, unaweza kupita kizuizi hicho cha kutokuamini sasa? Je, unaweza kumruhusu Roho Mtakatifu aingie sasa hivi na kuchukua mamlaka? Ikiwa unaweza, inaweza kutokea.

²¹⁰ Ugonjwa huo wa kisukari utakuacha, ikiwa utaamini. Nenda zako na ushangilie.

²¹¹ Unawazia nini kuhusu hilo? Yeye ni Yungiyungi la Uwandani, Nyota ya Asubuhi.

²¹² Ikiwa utaamini kwa ajili ya ugonjwa huo wa upungufu wa damu, utakuacha. Unaamini? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Nenda zako, shangilia, basi.

²¹³ Unaamini? Hebu tuamini kwa moyo wetu wote.

²¹⁴ Kama unaamini, nenda ukale chakula chako cha jioni. Hicho kidonda kilichokuwa tumboni mwako kimekuacha. Nenda, ule, na uamini.

²¹⁵ Ikiwa unaamini, haitakulazimu kufa. Kansa hiyo imekuacha. Unaamini? Nenda ukashangilie.

²¹⁶ Ni wangapi wanaoamini kwa moyo wenu wote? Simameni kwa miguu yenu sasa hivi. Simameni kwa miguu yenu, upesi sana. Inueni mikono yenu, vema, na kwa Mungu.

²¹⁷ Sasa, kwa nia moja, piteni kila kizuizi. Aminini ya kwamba Mungu yuko hapa, na maradhi na magonjwa yataondoka. Kila mtu, omba kwa njia yako mwenyewe.


²¹⁸ Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, sasa ninaleta hili Kwako, kusanyiko hili la watu. Ninamhukumu ibilisi. Ninadai kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yupo.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia kila roho chafu ya mashaka, ushirikina, kutokuamini, na dhambi, ziondoke kwenye jengo hili.

Toka, Shetani. Nakuapisha kwa Yesu Mwana wa Mungu.

²¹⁹ Kila mmoja wenu wekeaneni mikono sasa, na mwombeane, kila mahali humu jengoni, naye Mungu atawaponya. Amini kwa moyo wako wote. Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi, anzeni kuombeana. Ndivyo hivyo. Hiyo ndiyo njia.

²²⁰ Wote wanaoamini ya kwamba mmeponywa, inueni mikono yenu na kumsifu Mungu.

Vema, Ndugu Neville. 

58-1003 Kuangalia Yasiyoonekana
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org